# Haki za Ardhi za Wanawake na Jamii: Kuwekeza katika Wasaidizi wa Jamii katika masuala ya jinsia na ardhi

Ripoti ya Mkutano kwa Njia ya Wavuti





Kwa zaidi ya miaka mitano, Mradi wa Usalama wa Umiliki wa Ardhi kwa Wanawake (WOLTS) umekuwa ukichunguza uhusiano wa kijinsia na ardhi katika jamii za wafugaji zilizoathiriwa na uchimbaji wa madini Mongolia na Tanzania. Lengo limekuwa ni kutengeneza mbinu ya ushiriki wa jamii kwa muda mrefu na kujenga uwezo wa kulinda na kusaidia haki za ardhi za watu wote walio katika mazingira magumu  na hivyo kuelekeza nguvu katika usawa wa kijinsia, usimamizi na umiliki wa ardhi kwa mfumo ambao utarahisisha maboresho katika haki za ardhi kwa jamii yote.

Mradi umeonyesha kuwa kuwekeza katika kundi la wasaidizi wa jinsia na ardhi, wanawake na wanaume, inaweza kuleta mabadiliko makubwa kwa wanawake na jamii kwa ujumla.. Wasaidizi hao waliopata mafunzo kupitia mradi wa WOLTS wanaimarisha mifumo ya utawala kwenye ngazi ya jamii ili kuimarisha na kulinda haki za wanawake na makundi mengine yaliyo katika mazingira magumu na kuboresha haki za ardhi kwa wanawake na jamii. Hadi sasa, ushahidi unaonyesha kuwa mbinu ya WOLTS (kuwekeza katika wasiadizi wa jinsia na ardhi) inaweza kusaidia kuiwezesha jamii kupambana na kanuni za mifumo dume na kuleta mabadilko katika unyakuzi wa ardhi kwa nchi zinazoendelea. Katika jamii za majaribio, mbinu ya WOLTS ilifichua fursa za uongozi kwa wanawake, mabadiliko ya kanuni za kijamii ndani ya kaya, na kuongeza ufahamu wa unyanyasaji wa kijinsia.

Katika mkutano huo kwa njia ya wavuti, kiongozi wa timu ya WOLTS, Elizabeth Daley, alitoa muhtasari wa mradi huo, matokeo yake na uwezekano wa kutumiwa katika maeneo mengine. Michael Taylor, Mkurugenzi wa International Land Coalition, alizungumzia mtazamo wa ulimwengu juu ya uwezekano wa mradi kuchangia utawala bora wa ardhi kwa mabilioni ya watu wanaotegemea haki za ardhi zajamii. Washiriki waandamizi wa timu ya WOLTS, Joyce Ndakaru (HakiMadini, Tanzania) na Narangerel Yansanjav (People Centered Conservation, Mongolia) walitoa mifano kutoka nchi zao juu ya matokeo chanya ya kufundisha wasaidizi wa jamii juu ya masula ya jinsia na ardhi, na matumizi mapana ya matokeo ya mradi huo hadi sasa.

**Mwenyekiti:**

- **Christopher Tanner, Mokoro**

**Wawasilishaji:**

- **Elizabeth Daley, Mokoro**
- **Michael Taylor, International Land Coalition**
- **Joyce Ndakaru, HakiMadini**
- **Narangerel Yansanjav, People Centered Conservation**

**Rekodi ya mkutano kwa njia ya wavuti inapatikana hapa:**

**https://youtu.be/Grn83dokfH0**

## Jumbe Muhimu

- Ushiriki wa wanawake katika usimamizi wa ardhi umeongezeka
- Kuwekeza katika haki za ardhi kwa wanawake, kunalinda haki za ardhi kwa jamii
- Uelewa wa sheria zinazohusiana na ardhi na jinsia umeongezeka kwa karibu 50%
- Athari kubwa juu ya unyanyasaji na kanuni kandamizi za kijinsia
- Uwezeshaji wa wanawake kiuchumi –matokeo chanyayasiyo ya moja kwa moja
- Mbinu iliyothibitishwa - tayari kuigwa/kuendelezwa

Kwa muda mrefu, mradi wa WOLTS umejikita katika kushirikisha jamii na viongozi ili kuhakikisha umiliki wa mradi. Programu ya mafunzo ya wasaidizi wa jinsia na ardhi kupitia mradi wa WOLTS ulitanguliwa na miaka miwili ya utafiti wa awali na ushirikishaji wa kina katika kila jamii ili kupata misingi ya ushahidi. Programu hiyo ilitengenezwa kwa muundo unaoweza kuigwa ambao ulijumuisha na kukidhi mahitaji ya jamii husika. Kuanzia mwanzo wa mradi wa WOLTS, wanaume na wanawake wameshiriki kwa pamoja na kwa usawa. Timu ya WOLTS ilitengeneza mazingira salama na wezeshi kwa wasaidizi wa jinsia na ardhi ili kuongeza kujiamini kwa mtu mmoja mmoja na kama kikundi, wakitumia mbinu shirikishi katika vikao mbalimbali. Kuwekeza katika haki za wanawake za ardhi kunalinda haki za ardhi za jamii. Wasaidizi wa jinsia na ardhi waliofunzwa, sasa wanasaidia serikali zao za mitaa/vijiji kulinda maliasili kwa kuzingatia usawa wa kijinsia.

**HAKI ZA ARDHI KWA WANAWAKE NA JAMII**

**KUWEKEZA KATIKA WASAIDIZI WA JAMII**

*Matokeo ya miaka mitano ya kwanza ya Mradi wa Usalama wa Umiliki wa Ardhi kwa Wanawake (WOLTS)*

**Matokeo Muhimu:**
*Kufundisha wasaidizi wa jamii katika masuala ya jinsia na ardhi kuna faida kubwa kwenye jamii ikiwa ni pamoja na kupunguza unyanyasaji wa kijinsia*

# Muhtasari wa Mkutano wa Wavuti

## 1) JE! MRADI WA WOLTS KUPITIA PROGRAMU YA MAFUNZO KWA WASAIDIZI WA JINSIA NA ARDHI UMEPELEKEA MATOKEO GANI?

- Wasaidizi wa jinsia na ardhi wanawake, wameongeza kujiamini na hivyo wanachangia katika mikutano na wanaungwa mikono na viongozi wa mila katika kufanya hivyo.
- Wanawake wengi pia katika vijiji vya mradi waliwania nafasi mbalimbali za uongozi na walisaidiwa sana na wasaidizi wa jinsia na ardhi wanaume, haswa nchini Tanzania.
- Kuwekeza katika haki za ardhi za wanawake pia kunalinda haki za ardhi za jamii kwa hivyo ni "ushindi kwa pande zote" na sio "ama/au". Wasaidizi wa jinsia na ardhi nchini Mongolia wanaongoza juhudi za jamii kuziwajibisha kampuni za uchimbaji madini, kulinda ardhi kutoka kwa wawekezaji, na kusaidia serikali za mitaa katika uundaji wa kanuni mpya na upangaji unaozingatia usawa wa kijinsia.

## 2) JE! MBINU YA WOLTS INAFAA VIPI KATIKA MUKTADHA WA ULIMWENGU NA KUWAWEZESHA WANAUME NA WANAWAKE KULINDA HAKI ZAO ZA ARDHI?

- Ulimwenguni, kwa sasa kuna haja ya dharura ya kuongeza utambuzi wa haki za ardhi, hata hivyo, tuna ushahidi mdogo sana kwamba tunaelekea kwenye malengo kama vile Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals)
- Je! Tunawezaje kuendeleza mbinu ya mradi kwa njia ambayo itaepusha madhara katika kulinda haki za ardhi za jamii? Mradi wa WOLTS unaonyesha kuwa tunaweza kufikiria juu ya kuendeleza mbinu hiyo kutoka chini ambapo haki za walio hatarini zaidi zinaweza kupatikana kama sehemu ya juhudi za jamii.
- WOLTS ni mfano wa mradi wa kujenga demokrasia kutoka ngazi ya jamii ambapo wanawake, wanaume na vijana wanaweza kuamua maisha yao ya baadaye, wakianza na haki za ardhi ambazo ni msingi wa kuunda fursa mpya.
- Kulinda haki za ardhi za wanawake ni hatua moja katika kushinda ubaguzi mpana dhidi ya wanawake. Kuhimiza uongozi kwa wanawake kuna faida za muda mrefu katika nyanja nyingi za usawa wa kijinsia katika ngazi ya jamii.

## 3) JE! TIMU YA WOLTS IMEWEZAJE KUPIMA KUONGEZEKA KWA MAARIFA NA UFAHAMU WA SHERIA MUHIMU ZA ARDHI NA JINSIA KATI YA WASAIDIZI WA JINSIA NA ARDHI?

- Kwa kutumia tafiti za mtazamo, timu ya WOLTS iligundua ongezeko la karibu 50% katika viwango vya uelewa wa kisheria baada ya mafunzo. Ongezeko la jumla la mwamko wa sheria kati ya wasaidizi wa jinsia na ardhi wanawake lilikuwa 62%, na kati ya wanaume ilikuwa 37%.
- Kufundisha wawakilishi wa jamii wanaume na wanawake kuhusu ardhi na jinsia, inapelekea mabadiliko makubwa katika jamii, hii ni pamoja na mabadiliko katika mitazamo na tabia juu ya unyanyasaji wa kijinsia na uwezeshaji wa kiuchumi.

**4) JE! MRADI WA WOLTS UMELETA MABADILIKO GANI YA KIJINSIA NCHINI MONGOLIA NA TANZANIA?**

- Kupitia mazoezi mbalimbali kama vile michezo ya kuigiza, masuala yanayohusu unyanyasaji wa kijinsia yalianza kuibuliwa waziwazi na wawakilishi wa jamii walioshiriki katika mafunzo.
- Katika nchi zote mbili za mradi Mongolia na Tanzania, wanaume haswa wenye umri mdogo wameanza kushiriki katika majukumu ya nyumbani ambayo kijadi yalionekana kama majukumu ya wanawake. Utafiti kutoka Tanzania ulionyesha kuwa mara nyingi wanawake walilazimika kutoa viti vyao kwa wanaume wakati wa vikao, hata hivyo wasaidizi wa jinsia na ardhi wanawake na wanaume, wanahimiza kukomeshwa kwa vitendo hivyo, wakisisitiza kuwa ni ya kibaguzi.
- Nchini Mongolia, wasaidizi wa jinsia na ardhi wanatoa msaada mkubwa kwa wahanga wa unyanyasaji wa kijinsia. Mabango yaliyoorodhesha mawasiliano ya mawakala na mashirika ambayo hutoa msaada kwa waathiriwa wa Unyanyasaji wa Kijinsia (UWAKI) yamebandikwa karibu na jamii. Kwa kuongezea, wasaidizi wa jinsia na ardhi wamejaribu kuzingatia zaidi aina tofauti za unyanyasaji katika jamii na kuongeza uelewa, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa kihisia na kifedha, na masuala ya wanaume walio katika mazingira magumu.

**5) JE! MRADI WA WOLTS UMECHANGIA VIPI UWEZESHAJI WANAWAKE KIUCHUMI?**

- Programu ya mafunzo ya wasaidizi wa jinsia na ardhi wa WOLTS umejenga ujasiri kati ya wanawake ili kuweza kudai haki sawa. Mfano, nchini Tanzania, bei ya kuuza madini haswa madini ya vito (ruby na Tanzanite) imeongezeka kwa wanawake kutokana na ujasiri wa kuweza kupatania bei na hivyo kuwa sawa na bei ambayo wanaume hupokea. Pia kwa kuwataka waume wa wanawake wachekechaji kuwa wavumilivu na wenye subira ili wanawake waweza kuchagua kutouza madini yao wakati bei ni ndogo na kusubiri kupata bei nzuri.
- Huko Mongolia, mizozo ya ardhi huathiri maisha ya wafugaji ambao hutegemea ardhi kwa maisha yao. Wawakilishi wa jamii waliofunzwa sasa wanaweza kuwajibisha makampuni ya uchimbaji madini na kuwazuia kufanya uchimbaji ikiwa hawana leseni au ruhusa sahihi. Usalama juu ya ardhi umesaidia wafugaji kufanya kazi kwa ujasiri zaidi na kufanya shughuli za kuongeza kipato.

**6) JE! MRADI WA WOLTS UNA UMUHIMU GANI KAMA MBINU INAYOWEZA KUENDELEZWA/KUIGWA?**

- Nchini Tanzania, timu ya WOLTS imeona mahitaji kutoka kwa vijiji jirani ktaka kuiga programu ya mafunzo katika jamii zao.
- Mradi wa WOLTS umekwenda zaidi ya ngazi ya jamii nchini Mongolia kwa kushirikiana na Wakala wa Ardhi wa Serikali ya Kitaifa (ALAMGAC) kuandaa miongozo mipya ya kujumuisha kanuni shirikishi na usawa wa kijinsia ndani ya miongozo ya kitaifa juu ya mpango wa matumizi ya ardhi za vijiji. Hii inaonyesha kuwa mbinu za WOLTS zina uwezo wa kutoa matokeo chanya juu ya haki za wanawake za ardhi mbali na jamii za majaribio za mradi huo.

# Nukuu muhimu kutoka kwa Wanaharakati



"TIMU YETU ILIFANYA KAZI KWA BIDII KUTENGENEZA MAZINGIRA SALAMA NA YA KUSAIDIANA KATI YA WASAIDIZI WETU WA JINSIA NA ARDHI KUKUWA KATIKA KUJIAMINI, MMOJA MMOJA NA KAMA KIKUNDI, NA JAMBO HILI LA KUJENGA UJASIRI LILIKUWA JAMBO MUHIMU SANA KATIKA MCHAKATO WA WOLTS. TULIKUWA NA MAJADILIANO MENGI YA VIKUNDI. TULITUMIA MBINU ZA KUIGIZA; MIJADALA YA MAKUNDI YA JINSIA MOJA NA YA JINSIA ZOTE. TULIKUWA NA MAZUNGUMZO NA MAJADILIANO YA VIKUNDI VIDOGO –MJUMUISHO WA MBINU SHIRIKISHI. PIA TULICHUKUA HATUA YA ZIADA YA MAFUNZO KWAKURUHUSU MAONI KUCHIPUKA BILA MSUKUMO KUTOKA NJE."

**- ELIZABETH DALEY, MOKORO**



"TIMU YA WOLTS HAIPUUZI MVUTANO AMBAO UPO KATIKA NGAZI YA JAMII. PAMOJA NA HAYO YOTE, MRADI UMEWEZESHA MICHAKATO AMBAYO MAONI TOFAUTI NA MIVUTANO JUU YA HAKI ZA WANAWAKE ZA ARDHI NDANI YA JAMII ZINAWEZA KUSHUGHULIKIWA."

**- MICHAEL TAYLOR, INTERNATIONAL LAND COALITION**



"TULIPOANZA, WANAWAKE HAWAKUZUNGUMZA WALIPOKUJA DARASANI, HAWAKUCHANGIA, HAWAKUINUA MIKONO YAO HATA WAKATI WAKIWA NA HOJA. NI SEHEMU YA UTAMADUNI NA MILA WANAWAKE KUTOKUZUNGUMZA NA KUBISHANA MBELE YA WANAUME. TULIPOENDELEA KUJENGA UWEZO, KUHAMASISHA, NA KUJENGA UJASIRI, WANAWAKE HAO WALIANZA KUCHANGIA SANA KWENYE MIKUTANO. NA TUNAVYOZUNGUMZA LEO, WANA UJASIRI ZAIDI NA WANAWEZA KUCHANGIA SANA KWENYE VIKAO, HAWAWEZI KUACHA KIKAO KIISHE BILA KUCHANGIA CHOCHOTE. WAZEE WANAHIMIZA WANAWAKE KUSHIRIKI KATIKA MIJADALA NA KUSHIRIKI KATIKA KUFANYA MAAMUZI KWENYE JAMII."

**- JOYCE NDAKARU, HAKIMADINI, TANZANIA**



"WASHIRIKI WA MAFUNZO SASA WANAENDELEZA KIKAMILIFU HUDUMA KWA WANAWAKE WALIOATHIRIWA NA UNYANYASAJI WA KIJINSIA. KWA MFANO, MSAIDIZI MMOJA WA JINSIA NA ARDHI WA KIUME, ALITENGENEZA BANGO KUBWA LENYE MAWASILIANO KWA WAATHIRIKA WA UNYANYASAJI WA KIJINSIA KUOMBA MSAADA. ALIGUNDUA KUWA WANAWAKE MARA NYINGI HUSITA KUKARIBIA KWENYE BANGO DOGO KWA SABABU KILA WAKATI WALIFIKIRIA KWAMBA WANAWEZA KUTAMBULIWA AU KUONEKANA NA WENGINE KWA SABABU NI SUALA NYETI SANA. KWA HIVYO, BANGO KUBWA LINALONING'INIA KWENYE KUTA SASA LINAWEZA KUONEKANA NA KILA MTU. PIA, WASAIDIZI WA JAMII WA JINSIA NA ARDHI WANAUNGA MKONO JAMII ZAO KWA KUFANYA KAZI NA SERIKALI ZA MITAA/VIJIJI KWA NJIA SHIRIKISHI NA YENYE USAWA WA KIJINSIA. BAADHI YA MAGAVANA WA ENEO HILO WALITUAMBIA KUWA WASAIDIZI WA KIJINSIA NA ARDHI WANAWAKUMBUSHA KUZINGATIA MASUALA YA KIJINSIA WANAPOTENGENEZA KANUNI MPYA."

**- NARANGEREL YANSANJAV, PEOPLE CENTERED CONSERVATION, MONGOLIA**